

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI LUPOTO,
S. L. P 677,
TUKUYU.
04/12/2020.

Kumb.Na. LSS/UT/VOL.1/20/01.

Jina la Mwanafunzi
S. L. P
.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUPOTO WILAYA
YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2021.**

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kijiunga Kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Lupoto mwaka 2021. Shule ya Sekondari Lupoto ipo umbali wa kilometra 07 kutoka HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE. Usafiri wa Pikipiki kutoka Katumba unapatikana katika kituo cha basi cha KATUMBA kwa nauli ya Tsh. 1,000 – 1,500/=. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba ukiwa na mzazi/ mlezi wako.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare za shule

1. Wavulana Suruali mbili

- (i) Moja rangi ya **Kijivu** kitambaa cha cotton.
- (ii) Ya pili rangi ya **Ugoro** kitambaa cha cotton zenyenye marinda mawili mifuko mitatu

N.B Suruali zote mbili zinashonwa na Mzazi na zisiwe za kubana. Angalia kiambatanisho (kitambaa kimeambatanishwa).

- 2. Mashati mawili meupe yenyenye mikono mifupi tetron.
- 3. Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili (2) visivyo na visigino virefu.
- 4. Soksi nyeupe na ndefu jozi mbili (2)
- 5. Mkanda
- 6. Sweta rangi ya **Kijivu** yenyenye umbo la **V**
- 7. Tai ya rangi ya kijivu na ya rangi ya ugoro

1. Sare Wasichana sketi mbili

- (i) Moja rangi ya **Kijivu** kitambaa cha cotton.
- (ii) Ya pili rangi ya **Ugoro** kitambaa cha cotton.

NB: Sketi zote zinashonwa na mzazi/mlezi, ziwe ndefu na za heshima (zisiwe za kubana). Kuhusu rangi, angalia kiambatanisho.

2. Mashati mawili meupe yenyenye mikono mifupi tetron
3. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili,
4. Viatu vyeusi jozi mbili (2) visivyo na visigino virefu.
5. Sweta rangi ya kijivu yenyenye umbo la **V** mbele
6. Tai ya rangi ya kijivu na ya rangi ya ugoro.
7. Watakahitaji kuvaahijabu wanatakiwa kuvaahijabu ndefu inayotosha kusetiri mwili wa atakayevaa. (rangi ya hijabu ni nyeupe).

2.2 VIFAA VYA MASOMO

Unatakiwa kuleta vifaa vya masomo kama ifuatavyo:-

- i) Madaftari makubwa (counter books) kwa masomo yote 11atakayosoma.
- ii) Kalamu za wino blue au nyeusi za kutosha
- iii) Kalamu za penseli
- iv) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)
- v) Kamusi ya Kiingereza (Dictionary)

2.3 VIFAA VYA MICHEZO:

WAVULANA

- i) Bukta moja rangi nyeusi
- ii) Raba jozi moja
- iii) Fulana (T-shirt) rangi nyekundu damu ya mzee yenyenye mikono mifupi.
- iv) Soksi za michezo jozi moja ziwe ndefu rangi ya bluu.

WASICHANA

- i) Bukta moja rangi nyeusi, Kigauni rangi ya njano
- ii) Raba jozi moja
- iii) Fulana (T-shirt) rangi nyekundu damu ya mzee yenyenye mikono mifupi.
- iv) Soksi za michezo jozi moja ziwe ndefu rangi ya bluu.

2.4 VIFAA VYA USAFI

- i) Fagio (hard broom)
- ii) Jembe na kwanja kwa wasichana, Jembe na panga kwa wavulana (Shule yetu ni ya mchepuo wa kilimo lazima aje na jembe lake mwenyewe.
- iii) Ndoo ya lita 10 moja.

2.5 CHAKULA

Chakula cha mchana kwa wanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni jukumu la mzazi.

N.B: Chakula cha mchana kwa mwanafunzi ni lazima.

2.6 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule ya Sekondari Lupoto inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule nzima
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaare sare ya shule wakati wote kulingana na utaratibu wa shule
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i) Kutunza mali za umma.
- j) Kutunza mazingira ya shule.

3.0 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- (i) Wizi
- (ii) Uasherati
- (iii) Ubakaji
- (iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
- (v) Kupigana au kupiga
- (vi) Kuwa mjamzito/kupata mimba
- (vii) Kutoa mimba
- (viii) Kusababisha au kumpa mimba msichana
- (ix) Kuoa au kuolewa
- (x) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (xi) Kudharau Bendera ya Taifa
- (xii) Kugoma, kuchochaea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (xiii) Kukataa adhabu kwa makusudi
- (xiv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/ walezi na jamii kwa ujumla
- (xv) Uvutaji wa sigara

- (xvi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yote yale yanayovunja sheria za nchi.
- (xvii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
- (xviii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- (xix) Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua kama kunywa sumu, n.k

3.1 VIAMBATANISHO NA FOMU ZA KUWASILISHWA SHULENI

- (a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical Examination Form). Hakikisha imejazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shulenii
- (b) Fomu ya Taarifa binafsi ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
- (c) Fomu ya kukiri kukubaliana na Sheria, Kanuni na Maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

4.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Kila mwanafunzi atatakiwa kufuata na kutekeleza sheria na kanuni zote za shule kama inavyotakiwa.

5.0 KUSAJILIWA

Kabla ya kuja shulenii unatakiwa kutimiza yafuatayo:

- (i) Kupimwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali. Fomu imeambatanishwa.
- (ii) Hakikisha unakuja na cheti cha kuzaliwa.

Kumbuka kuwa umebahatika kupata nafasi hii ya pekee kati ya maelfu ya wanafunzi waliofanya mtihani. Hivyo ni lazima kuitumia nafasi hii kwa faida yako na taifa. Kinachokuleta katika shule hii ni kujifunza na kuelimika. Hivyo, unatakiwa kudumisha heshima na sifa ya shule hii ya Lupoto.

Unapofika ripoti kwa mwalimu wa zamu au makamu wa mkuu wa shule au kwa mkuu wa shule hii ili upewe maelekezo zaidi.

TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEKEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI LUPOTO

.....

**MKONG'OLA, ELIUTER
MKUU WA SHULE.**

SIMU: 0755 766641/0717 255353/0785 674477

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI LUPOTO
FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

SEHEMU A.

1. Jina la mwanafunzi
 2. Tarehe ya kuzaliwa..... Kabilia.....
 3. Jina la mzazi/ mlezi
 4. Uhusiano Kazi yake
 5. Anuani ya mzazi/ mlezinamba ya simu
 6. Mahali anapoishi mwanafunzi
- Umbali kuja shulenii ni kilometra.....

Majina ya Ndugu /Mlezi mwingine wa karibu

NA.	JINA LA NDUGU/MLEZI	UHUSIANO	NAMBA YA SIMU
1			
2			
3			
4			

7. **MENGINEYO** (Kama mgonjwa, yatima, mlemavu)

SEHEMU B:

TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUPOTO

Mimi
nimezisoma na kuzielewa Sheria, Kanuni na Taratibu za shule na kwamba niko tayari/siko tayari kuzifuata.

Sahihi ya mwanafunzi Tarehe

SEHEMU C: TAMKO /AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi ambaye ni
mzazi/mlezi wa mwanafunzi ninaahidi
kwamba nitatekeleza/sitatekeleza maagizo na mahitaji yote muhimu ya shule kama
nilivyoelekezwa na kwamba niko tayari / siko tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika
suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu ili kuinua Taaluma na Nidhamu yake.

Sahihi ya Mzazi/mlezi Tarehe